11. Ni kwa nguvu gani ndani yetu tunaweza kukabiliana na majaribu, na tunapigana na nguvu zipi? Waefeso. 6: 10-12.
12. Ni nini ngao yetu na ulinzi wetu? Waefeso. 6:16, 17.
13. Je, mateso na majaribu tunayoshinda kwa imani yana thamani yoyote? 1 Pet. 1: 7, 8, 9.
14. Wakati imani yetu ni halisi, tutatumiaje talanta zetu na maisha yetu, na matokeo yake ni nini? Mathayo. 25:20, 21.

*****************************

### Somo la Juni 20, 2026 (Tamuz 5, 5786)
## WAVUVI WA WATU

**Somo Kuu: Yohana 15:1-19.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:16.**

1. Je, Masihi anasema atawafanya nini wale anaowaatumia kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu? Mt. 4:19.
2. Je, mitume walikuwa na mafanikio ya aina gani ya uvuvi Mwokozi alipokuwa hayupo nao? Yohana 21:3-5.
3. Je, aliwaambia watupe wapi nyavu zao, na walipata mafanikio gani walipotii maelekezo Yake? Mstari wa 6.
4. Je, tunaweza kufanya kiasi gani cha kuvua watu bila Mwokozi kuwa nasi? Yohana 15:5.



11. Je! Matokeo ya kufurahisha yalikuwa gani? Mstari wa 8-15.
12. Ni aina gani ya kazi ambayo tunafaa kudumu kufanya, Je! Itakuwa ya bure? 1 Wakor. 15:58.
13. Je! Kuna rekodi mbinguni ya kazi yetu, na sala zetu hapa duniani? Matendo 10: 1-4.

*****************************

### Somo la Aprili 25, 2026 (Zif 8, 5786)
## USHAHIDI WA UPENDO WA ELOHIM

**Somo Kuu: 1 Wakorintho sura ya 13.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 3:16.**

1. Je! Inasemekana Elohim ni nini? 1 Yohana 4: 8.
2. Je! Elohim alijidhihirishaje kwa ulimwengu? Yohana 3:16.
3. Jinsi gani ahadi ya kwanza ya mkombozi ilitolewa? Mwanzo 3: 15.
4. Je! Elohim alimzuiaje mwanadamu kuwa mtenda dhambi wa milele? Mwanzo 3: 22-24.
5. Je, Upendo wa Elohim ni mkubwa kiasi gani? Mithali 10:12.
6. Kwa nini kubadilishwa ni muhimu? Yakobo 5:19, 20.
7. Ni kwa nini Bwana mwema alileta mafuriko duniani? Mwanzo 6: 5-8.
8. Kwa nini Elohim aliiokoa Ninawi? Yona 3: 3-5





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Pili
2026

Ya
Aprili, Mei, Juni.
**(Aviv, Zif, Sivan, Tamuz)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**
**Jerusalem — Israel**

9. Kwa sababu Elohim aliwapenda Israeli, aliwafanyia nini, na waliwatendeaje wajumbe wake? 2 Nyakati 36: 14-17.
10. Wakati Daudi alikaa mbali na upendo wa Elohim, Elohim alifanya nini? 2 Samweli 12: 9-13.
11. Je! Yahshua alionyeshaje upendo wake kwa Petro? Luka 22:31, 32.
12. Ni baraka gani imeahidiwa kwa wale ambao dhambi zao zimefunikwa na Damu ya Mwanakondoo? Zaburi 32: 1, 2.

    **Maelezo**. Haiwezekani kabisa kufanya somo ambalo kwa upeo wake litaweza kuelezea upendo wa Elohim. Upendo wa Elohim hauelezeki na hauna mipaka. Nafsi inayoamini kila wakati bila kujali jinsi ilivyo dhaifu machoni pa mwanadamu, inakubaliwa na Bwana, ikiwa kwamba dhambi zao ziko chini ya Damu ya Mwanakondoo.

*******************************



**Somo la Juni 13, 2026 (Sivan 28, 5786)**

## IMANI NA USHINDI

**Somo Kuu: Warumi 10: 12-21.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 10:17.**

1. Imani hujaje? Warumi, 10:17.
2. Angalia kwamba Neno lilikuwa karibu katika siku za Musa, lakini hawakuwa na imani, Kumb. 30: 14-15.
3. Je, imani ilikuwa rahisi kupata siku za Paulo? Warumi 10: 8.
4. Ni andiko gani linaonyesha kwamba tunatakiwa kufanyia kazi imani yetu? Waebr. 2: 4, 10:38.
5. Je! Njia itakuwa wazi kama tutasonga mbele siku kwa siku na kuishi maisha ya imani? Mithali. 4:18.
6. Je! Abrahamu alionyesha imani yake kwa matendo yake? Mwanzo 22:12.
7. Yakobo anasema nini kuhusu imani na matendo? Yakobo 2:20, 26.
8. Ni jinsi gani imani hufanywa kuwa kamilifu? Yakobo 2:21, 22.
9. Ni jinsi gani ni vigumu kuwa wenye haki kwa nguvu zetu na juhudi zetu bila kutafuta na kupokea Roho? Yeremia. 13:23; Isa. 64: 6.
10. Ni nani tu anayeweza kututakasa kutoka kwa dhambi, na ni jinsi gani? Matendo 4:12; Luka 11: 11-13.



**Somo la Aprili 4, 2026 (Aviv 17, 5786)**

## UFUFUO WA MASIHI

**Somo Kuu: Mt. 28:1-15.**
**Fungu La Kukariri: Mt. 28:6.**

1. Je, Yahshua alijibu nini kwa wale waliotaka ishara kutoka kwake? Mt. 12:40.
2. Je, Bwana na Mwokozi wetu Yahshua Masihi alifufuliwa lini? Mt. 28:1-6.

    **Maelezo**. Hivyo tunaona kwamba alitimiza ishara yake moja kwamba alikuwa Masihi wa kweli. Alisulubishwa katikati ya juma, hivyo akasababisha dhabihu na sadaka kukoma (Dan. 9:27), naye alifufuka mwishoni mwa Sabato ilipokuwa inakaribia kufika (Kiyunani: kufika) siku ya kwanza ya juma.

3. Je, ziara nyingine zilifanywa katka kaburi Lake? Marko 16:1-6; Luka 24:1-12.
4. Je, Bwana wetu Yahshua alimtokea nani kwanza baada ya kufufuliwa? Marko 16:9.

    **Maelezo**. “Alifufuliwa” iko katika wakati timilifu na inamaanisha muda fulani uliopita. “Mapema siku ya kwanza ya juma” inasema wakati alimtokea Maria Magdalena. Mkomo unaonekana umewekwa vibaya kama

**Somo la Juni 6, 2026 (Sivan 21, 5786)**

## KUWEKWA WAKFU KWA MMASIHI

**Somo Kuu: Warumi 6.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 6:16.**

1. Ni wakati upi kulikuwa na mtu mmoja bora zaidi katika Biblia aliyejitolea kwa Bwana? 1 Samweli 1:20, 24-28.
2. Je, Daudi aliitwa akiwa kijana? 1 Samweli 16: 10-12.
3. Uzito wa ujumbe wa Paulo ulikuwa upi? Warumi 12: 1. Linganisha na 1 Petro 2: 5.
4. Jinsi gani utakaso unafaa kuwa mkamilifu? Luka 14:33.
5. Jinsi gani Masihi alikuwa amejitakasa kikamilifu kwa kazi Yake? Wafilipi 2: 7, 8.
6. Tumeshauriwa kufanya nini katika jambo hili? Wafilipi 2: 5.
7. Tunapaswa kuenenda jinsi gani kama WaMasihi? 1 Wakorintho 6:19, 20.
8. Kabla ya utakaso kamili kupatikana, ni lazima tupitie nini? Yohana 3: 3; Waebrania 9:13, 14.
9. Ni nani peke yake ambaye anaweza kuziondoa dhambi zetu? 2 Timotheo 2:21.
10. Dhabihu za Elohim ni zipi? Zaburi 51:17.
11. Tumehakikishiwa nini ikiwa tutajitakasa kwake Yeye? Warumi 8: 1-11.

*******************************



**Somo la Mei 2, 2026 (Zif 15, 5786)**

## ROHO MTAKATIFU

**Somo Kuu: Wagalatia 5.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 14:16.**

1. Ni ahadi gani ya thamani ambayo Yahshua aliwapa wanafunzi Wake muda mfupi kabla ya kusulubishwa kwake? Yohana 14:16, 17.
2. Yahshua alimpa jina gani lingine Msaidizi? Roho Mtakatifu huwafanyia nini waumini? Mstari wa 26.
3. Ingawa ametumwa kwa jina Lake, Roho Mtakatifu anatoka kwa nani? Yohana 15:26.
4. Yahshua alisema ni nini bora kwake kuliko yeye kubaki duniani? Yohana 16:7.
5. Je, ni kwa jinsi gani Bwana yuko tayari kutupa Roho Mtakatifu? Luka 11:13.
6. Je, tunapokea Roho Mtakatifu katika hali gani? Matendo 5:32; Wagalatia 3:14.
7. Roho Mtakatifu ana sehemu gani katika kuzaliwa upya? Yohana 3:5, 7; Tito 3:5.
8. Ni nini tunaonywa tusifanye? Waefeso 4:30.
9. Je, matokeo ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste yalikuwa nini? Matendo 2:41.
10. Daudi aliomba kwa ajili ya nini? Zaburi 51:11.

**Maelezo**. Masihi Yahshua ameahidi Roho Mtakatifu na ahadi ni yetu. Mwokozi





tunavyoona pia katika Matendo. 19:12. Alama za uandishi si sehemu ya msukumo wa kimbinguni, kwani maandishi ya kale hayakuwa na alama za uandishi.

5. Je, habari ya Yohana juu ya kuonekana kwa Bwana wetu Yahshua Masihi ni ipi? Yohana 20:1-6.
6. Je, kulikuwa na ziara nyingi zilizofanywa kwa kaburi kulingana na ripoti zilizotolewa na waandishi wa Injili? Luka 24:22-24.

**Maelezo**. Hapa tunagundua katika mstari wa 23 neno "pia" linaloonyesha kwamba makundi yote mawili ya wanawake hawa walikuwa kwenye kaburi na walikuwa "pia" wameona malaika. Kisha wengine walikwenda tena na kukuta "kama walivyosema." Kwa hivyo kuna ziara tatu zilizoandikwa katika masimulizi. Katika wakati wa msisimko mkubwa hivyo, inawezekana sana kwamba ziara nyingi zaidi zilifanywa kwa kaburi tupu.

7. Je, Yohana 19:31 inawezaje kuelezwa, inayosema alikuwa akining'inia msalabani kabla ya Sabato? Law. 23:4-7.

*******************************

anapokaa ndani yetu kwa njia ya Roho wake Mtakatifu, tutakuwa washindi wa nafsi kama Yahshua alivyokuwa, tukijitoa kuwapata waliopotea. Si kwa ufasaha au mantiki mioyo ya watu hufikiwa, bali kwa mvuto mtamu wa Roho Mtakatifu, anayefanya kazi kwa utulivu lakini kwa hakika katika kubadilisha na kukuza tabia.

*******************************

**Somo la Mei 9, 2026 (Zif 22, 5786)**

## ROHO MTAKATIFU (inaendelea)

**Somo Kuu: Yohana 14:12-26.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 16:13.**

1. Je, Roho Mtakatifu ni nani? Roho Mtakatifu atafanya nini? Yohana 14:26.
2. Je, Petro alisema nini kuhusu Roho Mtakatifu? 2 Petro 1:20, 21.
3. Je, kuna Roho wangapi wa haki? Waefeso 4:4.
4. Je, Roho Mtakatifu alidhihirishwa vipi siku ya Pentekoste? Mdo. 2:1-8.
5. Je, Paulo aliiambia nini kanisa kuhusu Roho Mtakatifu? 1 Tim. 4:1-3.
6. Je, Yohana alishauri WaMasihi wafanye nini? 1 Yohana 4:1.
7. Je, tunawezaje kujua kwamba tuna Roho wa kweli? Warumi 8:16; Yakobo 1:26, 27.



5. Tukisoma kwa dhati na kujifunza neno lililoandikwa, ambalo lilikuja kwetu kupitia kuongozwa kwa manabii watakatifu, ni nini itafanyika? Isaya 30:21; Warumi 10:8.

6. Je, hatua inayofuata ni nini? Matendo ya Mitume 3:19; 2 Wakorintho 7:10.

7. Ni kwa nani tunafaa kutubu dhambi zetu? Zaburi 32: 5; 1 Yohana 1:9.

8. Tutajua aje kwamba mtu aliyekuwa katika dhambi, ametubu na kugeuzwa katika njia na mwenendo mpya? Mathayo 3:8; Warumi 8:13.

9. Je, tutapata amani ya akili, na dhamiri zetu zitakuwa huru kutokana na hatia, baada ya hatua sahihi kuchukuliwa? Warumi 8:1.

10. Mtu ambaye amezaliwa tena atakuwa akiishi kwa ajili yake mwenyewe tu, au kwa wengine? Atakuwa mtumishi ambaye ana faida kwa Bwana, kwa kusaidia kupeleka ujumbe wa wokovu? Yohana 15:1, 2; Mathayo 25: 29, 30.

*******************************



**Somo la Aprili 11, 2026 (Aviv 24, 5786)**

## YAHSHUA AWATOKEA WANAFUNZI WAKE WASIPOMTARAJIA

**Somo Kuu: Marko 16:9-20**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:16.**

1. Je, Yahshua aliwapa wanafunzi wake amri gani kuhusu kuhubiri Neno? Marko 16:15; Mathayo 28:19; Matendo. 1:8.

   **Maelezo**. Tunaona katika mistari hii kwamba wanafunzi waliamriwa na Yahshua kufundisha Injili kwa mataifa yote, watu na lugha, katika dunia yote. Hadi wakati huo wana wa Israeli peke yao ndio Bwana alikuwa akishughulika nao.

2. Kabla ya Bwana kupaa mbinguni, wanafunzi walikuwa wamekusanyika wapi? Yohana 21:2-3.

   **Maelezo**. Petro alipaswa tu kutoa pendekezo na mara moja wale waliokuwa naye wakafuata. Tunapaswa kuwa waangalifu sana tunachopendekeza sisi kama WaMasihi, kwani sisi pia tuna ushawishi kwa wale walio karibu nasi.



9. Je, Bwana hutazama muonekano wa nje? 1 Sam. 16:7.
10. Je, ni lazima wale wanaomtumikia Bwana wapate moyo mpya? Yeremia 24:7.
11. Je, Yahshua alitoa maelekezo gani kuhusu moyo? Mathayo 5:8.
12. Je, ni nani peke yake anayeweza kuelekeza mioyo yetu? 2 Wathesalonike 3:5.

*******************************

**Somo la Mei 30, 2026 (Sivan 14, 5786)**

## WOKOVU

**Somo Kuu: 2 Timotheo 2**
**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 2:15.**

1. Je, mwenye dhambi ana njia moja tu ya kuepuka dhambi na adhabu yake? Matendo 4: 12.

2. Jinsi gani Masihi Yahshua anaweza kuwa wokovu wa mwanadamu kutoka katika dhambi? Wafilipi 2:6-9.

3. Ni toleo gani la ajabu Baba alimpa kila binadamu? Warumi 3:23-26; 5:15-21.

   **Maelezo**: Mtu hawezi kununua wokovu, wala hawezi kujitafutia, kwani ni zawadi ya bure ya mbinguni. Kwa kutumia muda wake mbele ya kiti cha enzi cha mbinguni kwa moyo na akili inayofikilia mambo ya juu pekee yaliyo matakatifu, kuyatamani kwa dhati, na kutafuta na kuyaomba hayo mambo, ni hakika kuyapata. Luka 11:11-13.

4. Jinsi gani tutapata imani inayohitajika ili kuamini katika mambo haya na kuyatafuta? Warumi10:17.



8. Je, kuna roho nyingine zaidi ya Roho Mtakatifu? Isaya 8:19.
9. Je, tunawezaje kujua kwamba sisi ni wana wake? Warumi 8:9.
10. Je, Roho Mtakatifu anapatikanaje? Luka 11:10-13.
11. Je, tutakuwa watumishi wenye faida, na matawi ya Bwana yenye matunda Roho atakapoishi ndani yetu? Yohana 15:4, 5.

*******************************

**Somo la Mei 16, 2026 (Zif 29, 5786)**

## SIRI YA NGUVU ZA ELOHIM

**Somo Kuu: Matendo 2: 1-47.**
**Fungu La Kukariri: Matendo 2: 46, 47.**

1. Baada ya Yahshua kufufuliwa na kabla ya kupaa mbinguni, aliwaambia wanafunzi wake wasubiri nini? Matendo. 1: 4.
2. Ni ahadi gani ambayo Yahshua alisema watapokea? Mstari wa 5.
3. Je! Wanafunzi walijazwa na nini wakati ahadi ya Baba iliwajia? Matendo 2: 4.
4. Kama matokeo ya Nguvu zote za Elohim kupitia roho mtakatifu, ni jambo gani la ajabu lililotokea? Matendo 2:41.



wito "...Nifuateni, nami nitawafanya muwe wavuvi wa watu."

*******************************

**Somo la Juni 27, 2026 (Tamuz 12 , 5786)**

## IBADA YA MOYO

**Somo Kuu: Kumbukumbu la Torati 6.**
**Fungu La Kukariri: Kumb. 6:4, 5.**

1. Je, Bwana anahitaji ibada ya moyo kutoka kwa watu Wake? Kumb. 6:4, 5.
2. Je, baraka za kidunia zinafuata wale wanaomtafuta Bwana kwa moyo wao wote? Mstari wa 3.
3. Je, tukihitaji Neno Lake, na kutafuta kwanza ufalme wa Bwana na haki Yake, baraka nyingine zitafuata? Mathayo 6:33.
4. Tukimtafuta kwa mioyo yetu yote, nini kitakaa ndani yetu? Isaya 26:3.
5. Je, Yahshua alisema amri ya kwanza ni ipi? Mathayo 22:37, 38.
6. Je, vitu gani vinatoka moyoni? Mathayo 12:35.
7. Je, tunapaswa kulinda midomo yetu na ndimi zetu ili mazungumzo yetu yapendeze Bwana? Mathayo 12:36, 37.
8. Je, mwanasheria fulani aliyemjaribu Yahshua alijua kweli kweli Bwana anahitaji nini kutoka kwa wanaomtumikia? Luka 10:27.



3. Je! Ni nini kinachothibitisha kwamba Bwana hakupendezwa na walichokuwa wakifanya? Yohana 21:3, sehemu ya mwisho.
4. Je! Ni nani aliyeonekana ufuoni? Yohana 21:4.
5. Ni nini kilichotokea walipotii amri ya Bwana? Yohana 21:6.
6. Je, tunaweza kutimiza kitu chochote bila Yeye? Yohana 15:5.
7. Je, Yahshua alimuliza Petro swali gani lenye kugusa moyo? Yohana 21:15.
8. Je, Petro alihisi vipi Bwana alipomuliza mara ya tatu kama alimpenda kweli kweli? Yohana 21:17.
9. Petro alipoona mwanafunzi aliyependwa na Bwana akifuata, alimwuliza Bwana nini? Yohana 21:20-21.
10. Angalia jinsi Bwana alivyomwambia Petro asimwangalie mtu mwingine yeyote, bali kumfuata Bwana bila kujali mambo yote mengine. Yohana 21:22.

    **Maelezo**. Tunaweza kutazama kandokando kama Petro alivyofanya na kumwangalia mtu mwingine, kama Petro alivyowatazama wale waliokuwa wamesimama karibu. Ili kumpendeza Bwana wetu, hatustahili kujishughulisha na watu wanaotuzunguka, bali tusikie mafundisho, na kumfuata Bwana katika mambo yote. Waefeso 5:1.

*******************************

5. Wanafunzi wa Masihi walikuwa katika hali gani wakati Pentekoste ilipofika na Roho Mtakatifu akapeanwa? Matendo 2: 1
6. Je, Ni kazi gani nyingine za ajabu zilifanywa na nguvu za Elohim? Matendo 3: 1-8.
7. Je! Miujiza ambayo ilifanywa na mahubiri ya mitume ilikuwa na athari gani kwa wale walioshuhudia jambo hili? Matendo 4: 4.
8. Je! Kundi lote liliinuaje sauti zao kwa Elohim? Mstari wa 23-30.
9. Je! Matokeo ya maombi yao ya umoja yalikuwa nini? Mstari wa 31.
10. Je! Ni nini imesemwa kuhusu hali ya umati wakati huu? Mstari wa 32.
11. Je, matokeo ya umoja huu wa nia yalikuwa nini? Mstari wa 33.

******************************

**Somo la Mei 23, 2026 (Sivan 7, 5786)**

## MUUJIZA WA KUONGOKA

**Somo Kuu: 2 Wakorintho 5.**
**Fungu La Kukariri: 2 Wakorintho 5:17.**

1. Je, moyo wa binadamu unaelezwaje? Yeremia 17:9.
2. Je, ushahidi wa dhambi unaweza kuonekana moyoni mwa mtu? Yeremia 17:1.



3. Je, Mtume Paulo anaeleza vipi hali ya binadamu? Warumi 3:10-18.

**Maelezo**. Hii ni hali ya binadamu kwa asili yake. Kama kutakuwa na mabadiliko basi muujiza lazima ufanywe.

4. Je, kutowezekana kwa kujibadilisha wenyewe kunaelezwaje? Yeremia 13:23.
5. Je, Elohim kupitia Ezekieli anaeleza vipi kuhusu moyo wa mtu kubadilishwa? Ezekieli 36:24-26.
6. Baada ya mabadiliko haya kufanywa, na Roho wa Elohim kuingia, itakuwa na athari gani juu yetu? Mstari wa 27.
7. Je, mtenda dhambi anapaswa kufanya nini ili kupata msamaha? Mithali 28:13.
8. Je, kanuni hii inasisitizwaje katika Agano Jipya? Matendo. 2:38; 3:19.
9. Je, ni nini kinachothibitisha muujiza wa kuongoka? Wagalatia 5:22, 23.

******************************



**Somo la Aprili 18, 2026 (Zif 1, 5786)**

## THAWABU YA KUMKUBALI YAHSHUA

**Somo Kuu: Mat. 19: 23-30.**
**Fungu La Kukariri: Mat. 16:27.**

1. Je! Thawabu itakuwa gani kwa kuacha yote na kumfuata Yahshua? Mat. 19: 27-29.
2. Ni nini ingine inahitajika ili kupokea thawabu hii? Mat. 10: 37-39.
3. Je! Kazi yetu kwake ni lazima iwe kubwa? Mstari wa 42.
4. Je! Kuna ukomo juu ya kile tunaweza kufanya? 1 Wakor. 3: 6, 7.
5. Ni nani basi mfanyikazi mkuu pamoja nasi? Mstari wa 8 na 9.
6. Ni onyo gani limetolewa kuhusu kazi yetu na Masihi Yahshua? Mstari wa 10.
7. Je! Mtu anapaswa kufikiria kuanza kazi yake kibinafsi? Mstari wa 11.
8. Je! Ni faida gani katika kufanya kazi iwe ya kudumu? Mstari wa 13, 14.
9. Je! Ni maonyo gani mengine yaliyopewa katika sura hii kuhusu jinsi tunavyomfanyia kazi? Mstari wa 18, 19, na 21.
10. Je! Ni ni maneno gani ya kutia moyo ambayo nabii Azaria alimpa Mfalme Asa wakati mmoja? 2 Nya. 15: 1-7.



5. Je, tunaelezwa tuwe na mwenendo upi kwa wale tunaojaribu kuwafundisha? 2 Tim. 2:24.
6. Je, tunapaswa kuwaelimisha vipi? Mstari wa 25.
7. Je, Paulo anataja nini kama jambo la kwanza analoogopa kulikuta kati ya Wakorintho? 2 Wakorintho 12:20.
8. Je, mtume anataja mjadala kuhusiana na nini?? Warumi. 1:29, 31.
9. Je, anasema wale wanaofanya mambo kama hayo wanastahili nini? Mstari wa 32.
10. Je, hekima inayoshuka kutoka juu inaelezwaje? Yakobo 3:17, 18.
11. Je, tunapaswa kujibadilisha vipi kulingana na aina mbalimbali za watu ili kuwaokoa? 1 Wakorintho 9:19, 22.
12. Je, Mtume Paulo anasema tunapaswa kuwa nini kwa wale tunaoishi kati yao? 1 Tim. 4:12.
13. Je, tunaweza kuwa wavuvi wafanikifu wa watu, kwa nguvu na hekima zetu wenyewe? Zak. 4:6.
14. Ili kutupa wavu upande sahihi, katika kazi ya injili, tunapaswa kukaa ndani ya nani na kumfuata kwa makini? Yohana 15:4, 5.

**Maelezo**. Tusikie Neno la Elohim katika 2 Tim. 2:15, “Jitahidi kujionyesha umekubaliwa na Elohim, mtenda kazi asiye na aibu, akigawa kwa usahihi neno la kweli.” Tunaomba sote tusikie